# 21 MUNGU AMCHAGUA DAUDI

***Mungu amejitafutia mtu aupendezaye moyo wake***

**Lengo**:kuonyesha kwamba huanglia moyo naye hahukumu kwa maumbile ya nje.

UFUPISHO
Sauli hakudhibitisha kuwa mfalme mwaminifu (mwenye imani). Hakuamini kwamba Mungu alimaanisha kila alilosema. Hivyo mungu akmchagua mtu mwingine kuwa mfalme badala yake-mtu aliye mpenda Mungu na kumtii.1Samweli 16:1-13.

**MUNGU ACHAGUA MFALME AFAAYE.**
Kwa kuwa Israelilitaka kufanana na mataifa mengine<walikuwa wameomba Mfalme. Mungu aliwaruhusu kupata walichoomba na kuwapa Sauli. Alikuwa ni aina ya mfalme waliyemtaka-mrefu ,mwenye nguvu na mzuri wa umbile. Kuonenekana kwake kuliwapendeza watu lakini Mungu anayeona moyoni na akilini, aliona jinsi hasa alivyokuwa-mchoyo, mwenye kiburi na asiyejutia madhaifu(mapangufu) haya yaliyomfanya Sauli asifae kutawala watu wamungu. Kwahiyo Nabii wa Mungu Samweli alimwambia , BWANA ameurarua ufalme wa Israel kotoka kwako leo na amempatia mtu ambaye ni mwema (bora kuliko wewe(1samweli15:28) Haikuwa rahisi kwa samweli kumwacha Sauli.Alikuwa ameshajaribu kumsaidia na akasikitika(kuhuzunika) kwamba Sauli alishindwa. Lakini sasa Mungu alitaka ampake mafuta mfalme mpya. Tazama pembe yako ya mafuta alisema “nawe nenda nitakupeleka kwa Yese wa bethelehem, kwani nimejipatia Mfalme kati ya wanawe”kilembwe” (mjukuu wa mjuku) wa Boazi na Ruthu mwanamke aliyekuwa wa kabila la Yuda. Alikuwa na wana wanane, ambaye kitinda mamba (wamwisho mdogo) wao alikuwa Daudi (Rutha4:21-22;1samweli 16:11).

**MUNGU ALIMPELEKA SAMWELI BETHELEHEM 1Samweli 16:1-12.**
Hivyo samweli alienda Bethelehem kutoa dhabibu na akamwita Yese na wanaye kuja pia(1sam.16:2-5). Walipowasili Samweli alimwona Eliabu mwana wa kwanza wa Yese na akaona kuwa alikuwa mrefu na mzuri wa umbo”kwa hakika mpwakwa wa mungu yu mbele yangu”Samweli alifikiri (mstari 6)

Lakini alikuwa amekosea. Mungu alisema kwa Samweli, Usiangalie uso wake wala urefu wa mwili wake ; lakini BWANA huangalia moyo (mstari wa 7).Sita zaidi wa wana wa Yese ndipo walipopita mbele ya samweli,mmoja mmoja lakini Mungu hakumchagua yoyote kati yao. Kwa asilisamweli alitatizwa na kumwuliza Yese,”Je watoto wako wote wako hapa?” mdogo wao ndiye anakosekana kwani alikuwa nje akichunga kondoo. Yese aliambiwa kumwita. Yese alipomwita Daudi, Samweli aliona akiwa mwenye afya, mwenye macho mang’aavu, kijana mwenye kuonekana vyema. Mara moja Mungu akasema “ondoka, mpake mafuta kwani huyu ndiye” (mstari wa 12)

**MFALME MPYA APAKWA MAFUTA 1sam 16:13**
Daudi alikuwa kijana mdogo tu, lakini Mungu alimwangalia akikua hadi kuwa mwaminifu, mwenye mawazo na aliyejaa ujasiri. Aliujua moyo wake na kumchagua, kwa sababu alikuwa na karama zitazo mfanya Mfalme bora na mwenye hekima. Hivyo Samweli akainua pembe ya mafuta naye huku ndugu (kaka) zake Daudi wakiangalia, akampaka mafuta kuwa Mfalme wa Israel atakayefuata. Roho ya Yehova mara moja ikaja juu ya daudi na kudumu ndani yake kutoka siku ile. Hili lilionyesha walioshuhudia upako huo, kwamba Mungu alikubali alilolitenda samweli.ktk maatendo ya mitume 13:22 Mungu anatuambia ni kwanini alimchagua Daudi badala ya Sauli. “Nimempata Daudi mwana wa Yese, mtu aupendezaye moyo wangu, atakaye timiza mpenzi yangu yote” Daudi hakufanyika mfalme mara moja. Miaka ilibidi kupita kabla ya kuanza kazi kubwa ya kuwaongoza watu wa Mungu. Mungu alikuwa amemchagua na kumweka (kumtenga) kwa kazi ile kuu.

**SOMO KWETU**
Oh, nisomo kubwa kiasi gani kwa Samweli na kwetu sisi kwamba Mungu “huangalia roho” kwa kuwa Mungu anatutazama wote kama tulivyo.

**Lengo:**
Kuonyesha jinsi Daudi alivyopat nguvu kupitia imani yake kutoka kwa Mungu(au kmtegemea).

**UFUPISHO**
Maisha ya mchungaji wa kondoo, wakati wa Daudi yalikuwa ya upweke namara nyingine ya hatari. Ilimpasa kulinda makundi yake dhidi ya wanyama wa porini,na wakati huo huo (au vilevile) kuwaongoza kwenye malisho mazuri. Siku moja Simba alikuja na kuchukua mwana wa kondoo kutoka kundini mwa Daudi, wakati mwingine dubu alifanya hivyohivyo (1Samwe31 17:34-35). Lakini Daudi alimwamini Mungu kuweza kuwauwa wale wanyama wa porini kuokoa kondoo wake(zaburi 23). Mungu alimfunza Daudi kuweza kumtegemea kwa ulinzi na ndipo maana hakumuogopa hata Goliath (Samwel 17).

**CHANGAMOTO AU MAJIVUNO(MATUKANO) YA JITU LA WAFILISTI (1Samweli 17;1-11).**
Wafilisti walikuwa adui mda mrefu wa Israel. Katika siku ambapo samweli alikuwa mwamuzi Mungu aliisaidia Israel dhidi yao nao walipigwa (walishindwa) na kujikalia mbali na miji ya waIsrael, muda Fulani baada ya Samweli kumpaka mafuta Daudi,walakini, hawa wafilisti waliivamia Israel tena. Kwahiyo Mfalme Sauli alikusanya jeshi lake kuwahami watu wa Mungu dhidi ya adui zao. Jeshini walikuwapo wana watatu wa Yese. Majeshi hayo mawili yaliweka kambi kwenye mitelemko ya milima miwili yakikabiliana pembeni mwa bonde la gola. Mfilisti mkubwa sana kutoka gati aliyeitwa Golith, alijitokeza mbele ya jeshi la wafilisti kwa kuwatukana(kuwapa changamoto waisraeli ,Nayadharau majeshi ya Israeli leo” alipiga kelele, nipatieni mtu nitakaye pigana naye.

“Hasa,katika viliadi vya akilizetu, muhimu kiasi (jinsi) gani kuakikisha kwamba anachoona kinampendeza. Mungu anajua hata mawazo (ya ndani) ya mioyo yetu hata kama hatusemi choote juu yake (Zabuli139:1-2;44:21).hatuwezi kuficha mawazo au hisia.

Zetu kwake. Kama tunakumbuka hilowakati wote. Zitatusaidia kuwa wakweli nawenye haki katika njia zetu zote.

Wakati bwana yesu kristo ajapo duniani kuwa mfalme, atatuadhibu au kutupa. Tuzo kufuatana na iwapo mawazo na matendo yetu yamekuwa mabaya au mema (Ikoritho4:5). Hivyomambo tufanyayo. Kusema na kuwaza yote ni muhimu kama mawazo yetu ni mema maneno maneno yetu na matendo yatakuwa memafria (Tazamawali kwa mkufunzi Na9)

**Maelezo ya Nyongeza:**

Katika somo la 5 tuliona jinsi maisha ya musa yalivyo fanana na ya yesu kwa njia. Nyingi sana tunaona wakati Daudi anapochanguliwa kuwa mfalme kwamba maisha. Yake tokea mwazoni kabisa ni mfano wa maisha ya Bwana Yesu Kristo.

| | |
|---|---|
| Daudi alizaliwa Bethelehemu,wakabila la yuda 1samweli 16:/ | Yesu alizaliwa Bethelehemu “mji wa Daudi wa kabila yuda (luka 2:4:11) |
| Mungu alimtangaza Daudi kuwa mfalme juu ya Israelui kwa kuwapaka mafuta. (Isamweli 16:13) | Munguali mchangua yesu kuwa kristo na kumpaka kwa Roho mtakatifu alipo batizwa (yohana1:32;49) |

| | |
|---|---|
| Daudi alikuwa mchungaji wa kondoo (Isamweli 16:11) | Yesualikuwa"mchungaji mwana<br><br>(yohana 10:11) |
| Daudi alikuwa mtu aliye pendeza roho ya mungu (matendo 13:22) | Yesu alikuwa"mwana wa mungu nipendezwaye naye. (Luka 3:22) |

Tunapata mifano mingi zaidi kama huukatika masomo yafuatayo. Yanatusaidia kufahamu jinsi mungu alivyowafundisha watu wake kumngojea wakatiwote kwa masihi ajaye.

**MASWALI:**

**Majibu mafupi:**

1.Nani alikuwa mfaime wa kwanza wa Israeli?
2.Ni aina gani ya mtu alichanguliwa baada ya sauli kuwa mfalme?
3.Ni kwenye nyumba ya nani alikopelekwa Samweli ?
4.Je,yesu alikuwa na wana wangapi ?
5.Ni mwana yupi wa yesu mungu alimchagua ?
6. Samweli alijuaje ni mtoto yupi wa yesu ampake mafuta ?
7. Samweli alimpaka mafuta vipi Daudi ?
8. Je.Daudi alifanyika mfalme maza moja baada ya kupakwa mafuta?

**Majibu ya kina**

1. Eleza habali ya nini kilitokea mungu alipo mtuma mgumbani kwa Yesu
2. (a) Ni nini mungu anachoweza kukiona ndani yetu zaidi yatunavyoonekana kwa nje?
   (b) Ni aina gani ya mawazo yatupasa kufikiri?
3. (a) malizia nukuu zifuatazo –"kwani bwana haoni kama mwanadam aonavyo……"
   (b) Ni somo fungo gani kubwa tunajifuza kutoka hili?

**Majibu ya ziada:**

4) Ni kwa vipi maisha ya kwanza ya Daudi ni mfano wa maisha ya Bwana Yesu Kristo?

